

## Maswali

1. Akida wa Warumi aliishi wapi?
2. Akida wa Warumi alifanya Wayahudi nini?
3. Mbona Akida alikuwa na huzuni na wasi wasi?
4. Wayahudi waliuliza nani asaidie Akida?
5. Waliambia Yesu nini juu ya Akida?
6. Mbona Akida alifikiria kwamba hakustahili Yesu kukuja nyumbani kwake?
7. Akida alifanya nini ikiwa alitaka kitu chochote kifanyike?
8. Akida aliuliza Yesu afanye nini?
9. Mbona Yesu alishangaa?
10. Marafiki wa Akida walipata nini walipofika nyumbani mwa Akida?

## Majibu

1. Akida wa Warumi aliishi Kapernaumu.
2. Alikuwa amewajengea Sinagogi.
3. Alikuwa na huzuni na wasi wasi kwa sababu mtumwa wake ali-kuwa mgonjwa sana.
4. Wayahudi waliuliza Yesu asaidie Akida.
5. Walimwambia kwamba Akida alikuwa mtu mzuri aliyependa watu wao na hata alikuwa amewajengea Sinagogi.
6. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu na Akida alikuwa Mrumi.
7. Aliwambia watumwa wake wafanye hii au wafanye kile na walifanya.
8. Akida alimuuliza Yesu aseme neno tu, la kumponya mtumwa wake.
9. Yesu alishangaa kuona Mrumi akiwa na imani kubwa kama hiyo.
10. Walimpata Akida ana furaha kwa sababu mtumwa wake alikuwa amepona.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1 Mwaka wa 3**



## 41 Mtumwa wa Akida

### Marejeo

Luka 7:1—10

### Kiini cha somo


Kuonyesha vile Akida alikuwa na imani kubwa kwa Yesu kwamba atamponya mtumwa wake.

### Maneno maalum

- 41.1 Kapernaumu + Akida + mzuri na mkarimu + kanisa
- 41.2 Akida ana huzuni + mtumwa mgonjwa + Wayahudi + Yesu + utakuja?
- 41.3 Akida + Yesu Mwana wa Mungu + si mzuri sana + usikuje + sema neno tu + imani kuu
- 41.4 Marafiki wa Akida + Akida + mtumwa alipona + furahi

**41.1** Katika kijiji kimoja kidogo cha uvuo wa Kapernaumu kuliishi askari wa Kirumi aliyekuwa mkarimu sana. Hakukuwa askari wakawaida tu. Aliitwa Akida. Alikuwa afisa aliyesimamia askari 80. Askari wote walifanya yote yenze Akida aliaambia wafanye. Akida akiamrisha askari aende popote, yule askari alienda haraka. Akiaambia askari, "Fanya hivi," askari angefanya papo hapo. Askari wote walimpenda kwa sababu alikuwa mzuri tena mkarimu.

Wakati huu Wayahudi walikuwa wakiishi kwa nchi yao lakini walikuwa wanatawaliwa na Warumi. Wayahudi hawakupenda Warumi. Lakini huyu Akida alipendwa na Wayahudi kwa sababu alikuwa mzuri k w a o . A l i k u w a amewajengea sinagogi (Kanisa) kule Kapernaumu.



**41.2** Siku moja Akida alikuwa na huzuni na wasi wasi pia. Alienda kutafuta Wayahudi fulani. Aliwambia kwamba mtumwa wake alikuwa mgonjwa sana. Wayahudi walifikiri kwamba labda Yesu angemtibu mtumwa wa Akida.

Wayahudi walienda kumtafuta Yesu na wakamwambia, "Bwana mzuri, mtumwa wa Akida, rafiki wetu ni mgonjwa sana, hata anaweza kufa. Tafadhalii, kuja umsaidie awe mzima." Hawakuwa na uhakika kama Yesu angekubali kuja na asaidie mtu aliyekuwa Mrumi. Kwa hivyo walimwambia, "Yeye ni mtu mzuri na anapenda watu wetu. Alitujengea Sinagogi." Yesu aliwambia, "Nitakuja. Nionyeshe njia ya kwenda kwake."

**41.3** Akida alijua Yesu ni mtu mkuu sana. Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu. Akida aliona si vyema Yesu kukuja nyumbani kwake. Kwa hivyo alituma ujumbe kwa Yesu, "Bwana, tafadhalii usijisumbue kukuja kwangu kwa sababu mimi sifai kukutana na wewe. Mimi naweza kuambia mtumwa wangu "Enda," na anaenda ama kwa askari, "fanya hii," na anafanya. Unaweza kufanya hivyo kwa uwezo wako. Unatakiwa kusema neno tu na mtumwa wangu atapona, bila wewe kukuja nyumbani kwangu."

Yesu alishangaa kuona mtu aliyekuwa Mrumi anaweza kuwa na imani kuu kama hiyo. Na hali watu wake wenyewe hawakumwamini. Lakini huyu Akida, hakuamini tu kwamba Yesu anaweza kufanya huo muujiza peke yake lakini aliamini kwamba anaweza kumponya bila kwenda kumwona! Mtu aliye na imini kama hiyo alisitahili kusaidiwa. Alikuwa na imani kuu, awe ni Myahudi au ni Mrumi.

**41.4** Marafiki wa Akida walirudi nyumbani kwake na Yesu akaenda zake. Marafiki wa Akida walipokuwa wakiingia nyumbani mwake, Akida alikutana nao akitabasamu. Hakuonekana ana wasi wasi kama awali. Mtumwa wake aliyekuwa mgonjwa na karibu kufa muda mchache uliopita, alikuwa amepona kabisa. Mara tena Yesu alikuwa amemfurahisha mtu mzuri na mkarimu.

